

# Rasilimali za COVID-19

## Unyanyasaji Nyumbani Wakati wa Kutengwa:

Tunajua unyanyasaji na vurugu zinaongezeka wakati wa kutengwa. API Chaya iko wazi na imejitolea kutoa huduma. Tunajua watu wengi wanakaa nyumbani kwa muda zaidi, na wana ufikiaji mdogo wa jamii na rasilimali zingine kupitia kazi na ratiba zingine za kila siku (safari, ukumbi wa mazoezi, shughuli za kijamii, nk.). Tunajua afya yetu ya kiakili, kiroho na kimwili imeathiriwa na imeunganishwa. Tunajua kuwa jamii zenye walemavu zimekuwa zikiunda mitandao ya huduma na rasilimali kwa muda mrefu, na kazi yetu inaendeleza desturi hio.

## API CHAYA IMEFUNGULIWA

Tumehamisha shughuli za tunatoa huduma za mbali. Tunapatikana kwenye simu yetu ya usaidizi (1-877-922-4292) na simu ya ofisi (206-467-9976) kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, 10 asubuhi hadi 4 jioni.

Rasilimali za saa za baada ya kazi:

National Domestic Violence Hotline (Nambari ya Simu ya Kitaifa ya Unyanyasaji Nyumbani): 1-800-799-7233

King County Sexual Assault Resource Center (Kituo cha Rasilimali za Unyanyasaji wa Kingono cha Kaunti ya King): 1-888-998-6423

National Human Trafficking Hotline (Nambari ya Dharura ya Kitaifa ya Biashara ya Binadamu): 1-888-373-7888

Sisi kama jamii hebu tuendelee kutumia utunzaji wa pamoja kama desturi, tunatumai rasilimali hii inaweza kusaidia desturi hii.

## Usaidizi kwa Eneo la Biashara Zinazomilikiwa na Watu wa Asili ya Kichina/Biashara za Wilaya ya Kimataifa:

Chuki ya Wageni na unyanyapaa dhidi ya biashara za Waasia Wamarekani umekuwa ukikatisha tamaa ya watu kusaidia biashara na mikahawa midogo katika Maeneo ya Biashara Zinazomilikiwa na Watu wa Asili ya Kichina/Wilaya ya Kimataifa ya Seattle kwa miezi kadhaa sasa.

Baadhi ya wamiliki wa biashara wameripoti kupungua kwa biashara kwa 60%. Baadhi ya wamiliki wanalazimika hata kuchukua hatua ngumu za kuwafuta wafanyakazi au kufunga biashara yote.

Hatua za kutembelea na kusaidia biashara za AAPI ni kitu ambacho sisi sote tunaweza kufanya ili kusaidia wale walioathiriwa moja kwa moja na unyanyapaa dhidi ya chuki ya Waasia, haya yote kwa kula na kufanya ununuzi katika biashara zao za ajabu.

## Rasilimali za APA Labor Alliance:

Katika Jimbo la Washington, wafanyakazi wote wa umma wataendelea kulipwa wakati huu. Hata hivyo, bila sera za nchi zinazohakikisha kulipwa wakati wa likizo ya ugonjwa na mipango mwafaka ya bima ya afya kwa ajili ya wafanyakazi wote, watu wengi

wanaofanya kazi wanazuiwa kufuata mwongozo wa CDC wa kukaa nyumbani wakati wanaugua.

Angalia zana yetu ya APALA kwa ukamilifu hapa. Pia angalia raslimali za mkurupuko wa COVID-19 za AFL-CIO.

**Usaidizi wa Kiuchumi kwa Watu Binafsi: Usaidizi katika kujaza fomu kwa lugha:**

Chinese Information Service Center inaweza kukusaidia kujaza fomu na maombi muhimu ili kustahiki usaidizi kutokana na COVID-19. Tembelea ukurasa wao wa wavuti katika <https://cisc-seattle.org/covid19/> ili upate rasilimali au uwasiliane moja kwa moja na wafanyakazi ambao wanaweza kukusaidia!